

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
WIZARA YA MALIASILI NA UTALII

Telegrams" "MALIASILI"  
Tel: +255 26 2321514/2321568  
Barua pepe: [ps@mnrt.go.tz](mailto:ps@mnrt.go.tz)



Mtaa wa Kilimani  
Barabara ya Askari,  
S.L.P 1351,  
40472 DODOMA.

**TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI**

**MAENEO YA VIJJI NA VITONGOJI VILIVYOKO KATIKA MAENEO YA HIFADHI**

Naibu Waziri Wizara ya Maliasili na Utalii Mhe. Constantine Kanyasu, amewataka wananchi wote wanaovamia maeneo ya Hifadhi kuacha mara moja na kurejea katika maeneo yao ya awali.

Mhe. Kanyasu, amekemea vikali vitendo vya baadhi ya wananchi wanaovamia maeneo ya Hifadhi na kuingiza mifugo pamoja na kupanda mazao kinyume cha sheria na kuwataka kusubiri hadi hapo wizara husika zitakapolipatia ufumbuzi suala la vijiji na vitongoji 366 vilivyoainishwa kuwepo katika maeneo ya Hifadhi kulingana na taratibu.

Naibu Waziri Kanyasu amesisitiza kuwa, yeyote atakayekwenda kinyume na agizo hili atachukuliwa hatua kali za kisheria.

Hivi karibuni, kumekuwepo na taarifa za uvamizi wa makundi ya mifugo ndani ya Mapori ya Akiba na Misitu ya Hifadhi. Zipo taarifa kutoka maeneo mbalimbali kama Mapori Tengefu, Mapori ya Akiba na Misitu ya Hifadhi kuwa kuna wananchi wanaswaga mifugo na kuingiza ndani ya Hifadhi. Aidha, kumekua taarifa za maeneo oevu kuvamiwa na baadhi ya wananchi.

Naibu Waziri Kanyasu ameziagiza taasisi husika za Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyamapori Tanzania (TAWA), Mamlaka ya Hifadhi ya Bonde la Ngorongoro, (NCAA), Hifadhi za Taifa Tanzania (TANAPA) na Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania (TFS) kuendelea kuzuia uvamizi huo na kuchukua hatua za kisheria dhidi ya wavamizi bila ya kisingizio chochote.

Onyo hili limetolewa, kufuatia baadhi ya wananchi kuanza kuvamia maeneo ya Hifadhi kwa kuingiza mifugo na kupanda mazao kufuatia kutokuelewa vema maagizo yaliyotolewa na Mhe. Rais tarehe 15 Januari 2019 na kuanza kuvamia maeneo ya hifadhi badala ya kubaki katika maeneo waliyomo wakati wakisubiria ufumbuzi wa migogoro. Aidha, amebainisha kuwa si maeneo yote 366 yatakatolewa kwa wananchi.

Mnamo tarehe 15 January, 2019, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, aliziagiza wizara zote zinazohusika ( Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Ofisi ya Rais Ikulu, Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Wizara ya Maliasili na Utalii na Wizara ya Ardhi ) kusitisha mara moja zoezi la kuviondoa vijiji na vitongoji vinavyodaiwa kuwepo katika maeneo ya hifadhi na kuzitaka wizara zote zinazohusika kukutana ili kubainisha na kuanza mchakato wa kurasimisha maeneo ya vijiji na vitongoji hivyo.

Naibu waziri Kanyasu amefafanua kuwa, agizo la Mhe. Rais Dkt. John Pombe Magufuli, halikumaanisha kuwa sasa wananchi wanaruhusiwa kuvamia, kuingiza mifugo na kulima katika maeneo ya Hifadhi.



**Dorina G. Makaya**

**Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano Serikalini**

**27 January, 2019**